

## **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI MTIHANI WA TAIFA WA DARASA LA NNE - 2012**

● 055

### **SOMO: SAYANSI**

JINA LA MTAHINIWA: .....

JINA LA SHULE: .....

HALMASHAURI: .....

MKOA: .....

● MUDA: SAA 1

### **MAELEKEZO:**

1. Karatasi hii ina sehemu nne, A, B, C na D
2. Jibu maswali yote kama ilivyoelekezwa.
3. Majibu yote yaandikwe kwenye karatasi hii.
4. Kumbuka kuandika jina lako, jina la shule, halmashauri na mkoa.
5. Simu za mkononi haziruhusiwi kwenye chumba cha mtihani.

### SEHEMU: A

Jibu swali la 1 – 10 kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuandika katika kisanduku kilicho pembedni.

1. Baadhi ya ajali na maafa yatokanayo na nguvu za asili ni.

- A. Mvua kubwa, umeme, kimbunga
- B. Radi, kimbunga, mvua kubwa
- C. Umeme, madaraja, kimbunga
- D. Mitambo, mafuriko, miti

2. Wanyama wanaokula nyama wana:-

- A. Pembe ndefu na kali
- B. Mikia mipana na mifupi
- C. Meno makali na kucha kali
- D. Pembe kali na kucha kali

3. Mbu wanaosambaza vimelea vya malaria huuma:-

- A. Usiku tu
- B. Mchana tu
- C. Usiku na mchana
- D. Usiku wa manane

4. Zifuatazo ni njia za kumsaidia mtu aliyezirai isipokuwa moja. Ipi hiyo?

- A. Mweke mgonjwa katika sehemu salama yenye hewa ya kutosha
- B. Inua miguu ya mgonjwa kuruhusu damu iende kichwani
- C. Mvue viatu na kulegeza mkanda wake
- D. Kama hapumui umwagie maji ya baridi mwili mzima

5. Maji huganda katika nyuzi joto:-

- A.  $100^{\circ}$  C
- B.  $36^{\circ}$  C
- C.  $0^{\circ}$  C
- D.  $36.9^{\circ}$  C

6. Ili kugomboa chumvi katika maji ni lazima maji:-

- A. yachujwe
- B. yapozwe
- C. yachemshwe
- D. yagandishwe

7. Mikono ya (mishikio) ya pasi na vikaangio hutengenezwa kwa mbao kwa sababu:-

- A. Mbao hupendezesha pasi na vikaango
- B. Mbao ni kipitisho hafifu cha joto
- C. Mbao huharibika haraka
- D. Mbao ni kipitisho kizuri cha joto


8. Kipi kati ya vifuatavyo ni chanzo kisicho cha asili cha mwanga?

- A. Jua
- B. Radi
- C. Nyota
- D. Moto

9. Ni aina gani ya nguo haitokani na viumbi hai? Ni nguo za :-

- A. Nailoni
- B. Silki
- C. Pamba
- D. Sufu

10. Chunguza michoro ifuatayo kisha jibu swali lifuatalo



Kati ya michoro hii (i), (ii) na (iii) ni glopu ipi haitawaka?

- A. (i)
- B. (iii)
- C. (ii)
- D. (ii) na (iii)

### SEHEMU: B

Jibu swali la 11 – 17 kwa kujaza nafasi wazi

11. Hewa iliyo katika mwendo huitwa .....
12. Joto kutoka kwenye moto hufikia ngozi zetu kwa njia ya .....
13. Taswira ni matokeo ya kioo ..... mwanga.
14. ..... kinasambazwa na konokono kutokana na kukojoa na kujisaidia haja kubwa kwenye vyanzo vya maji.
15. Maji katika hali ya yabisi huitwa .....
16. Ncha za sumaku zinazotofautiana zikikaribiana.....
17. Kitendo cha mwanga kupinda unapotoka media moja kwenda nyingine huitwa ..... kwa mwanga.

### SEHEMU: C

Jibu swali la 18 – 20 kwa kuandika “KWELI” au “SI KWELI”

18. Hewa ya kaboni dayoksaidi inasaidia moto kuwaka.....
19. Chuma kinapopashwa moto hutanuka .....
20. Chembe chembe hai nyeupe husaidia kulinda mwili dhidi ya magonjwa ....

### SEHEMU: D

Jibu swali la 21 – 25 kwa kuoainisha fungu “A” na fungu “B” kwa kuweka herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopewa.

NA.	FUNGU: A	( )	FUNGU: B
21.	Sepali	( )	(a) Katika kinachoruhusu kiasi kidogo cha mwanga kupenya
22.	Fagio	( )	(b) Sehemu ya ua yenyre rangi huvutia wadudu na ndege
23.	Minyoo	( )	(c) Mashine rahisi daraja la tatu
24.	Mwangwi	( )	(d) Sauti iliyosharabiwa
25.	Angavudufu	( )	(e) Sehemu ya ua yenyre rangi ya kijani hulinda ua
		( )	(f) Mashine rahisi daraja la pili
		( )	(g) Kutumia choo kwa haja ndogo na kubwa
		( )	(h) Kuoga kila siku kwa maji safi
		( )	(i) Sauti iliyokisiwa
		( )	(j) Kitu kinachoruhusu mwanga kupenya